TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION (TARO)
(TAASISI YA HAKI ZA WASANII)
S.L.P 70624 Dar es salaam, Simu:+255785769223,+255767292581
Barua pepe:tarotanzania@gmail.com,Mitandao ya kijamiii:instagram/fb, taro.tz
Anwani ya Ofisi: Mtaa wa Kihonzile , Mkabala na Daraja la kuelekea Bagamoyo,
Kata ya Mabwepande , Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam
"Tunasimama kwa ajili ya Haki na Maslahi ya wasanii wote"

Ref.No: Taro /P/2022/ A04 **: Swahili Version:** Date: 11st February 2022

# MTAZAMO WA KISHERIA KUHUSU BASATA KUENDELEZA UBAGUZI KWA WASANII (DISCO JOKERS-DJS) KATIKA UANDAAJI WA TUZO ZA MUZIKI TANZANIA

Rejea kichwa cha habari hapo juu. **Tanzania Artists Rights Organization (TARO)** au kwa lugha ya Kiswahili **"TAASISI YA HAKI ZA WASANII"** ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiriwa na sheria ya Mashirika yasiyo ya kiserikali iitwayo **"Non Governmental Organization Act.No.24. of 2002"**, Mnamo tarehe **26/11/2021**. Lengo kuu la **TARO** ni kuiwezesha jamii ya kitanzania kushiriki kikamilifu katika kupambana na umasikini kwa kutumia sanaa na fasihi. Katika kuakikisha inafanikiwa kwenye lengo lake kuu tajwa, moja ya shughuli za TARO ni kusaidia kulinda haki na maslahi ya wasanii wote kuhusiana na kazi zao za sanaa.

Mnamo tarehe 28 mwezi Januari 2022, Baraza la Sanaa Taifa (BASATA) wakishirikiana na Copyright Society of Tanzania (Cosota) walifanya uzinduzi wa tuzo za muziki. Uzinduzi huo ulihudhuliwa na wadau mbali mbali wa muziki wakiwemo wasanii mbalimbali. Maswali ya sintofahamu yalibubujika kuhusiana na mchakato mzima wa kutoa mialiko kwa wasanii, ambapo baadhi ya wasanii walikosa mialiko hiyo na kuhoji kwanini hawakualikwa. TARO tulifanya uchambuzi wa kisheria kwenye mchakato mzima uliotumika kualika wasanii na kugundua uwepo wa vitendo vya **KIBAGUZI** kinyume na ibara ya **13(4)** ya **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)** kama inavyofanyiwa marekebisho mara kwa mara.TARO tulilaani vitendo vile vya Kibaguzi.

Mnamo tarehe 30 Januari 2022, Baraza la Sanaa Taifa (BASATA) walitoa rasimu ya vipengele vya **Tuzo za Muziki Tanzania** kwa ajili ya wasanii na wadau kujadili na kutoa maoni. Ambapo katika rasimu hiyo wasanii aina ya Disco Jokers(Dj's) walihusishwa katika kipengele chao.

Mnamo tarehe 11 Februari 2022 BASATA walitoa orodha ya vipengele vya kuwania **Tuzo za Muziki Tanzania**, katika hali ya kusikitisha, kipengele cha wasanii aina ya Disco Jokers(Dj's) kimeonekana kuondolewa katika tuzo hizo bila BASATA kutoa maelezo yoyote kwa umma juu ya maamuzi hayo.

Hali hiyo imelalamikiwa sana na baadhi ya wasanii wa aina hiyo ya Disco Jokers(Dj's) na kusababisha TARO kutafakari uhalali wa maamuzi hayo kisheria uliofanya na Baraza la Sanaa Taifa (BASATA) .

## HOJA ZA KISHERIA

**Je tuzo zimeandaliwa kwa ajili ya wasanii wa muziki wanaoimba tu.?**

Kwa mujibu wa vipengele mbalimbali vya tuzo za muziki vilivyoorodheshwa na BASATA mnano tarehe 09 Februari 2022 katika taarifa yao ya umma iliyotolewa na Katibu Mtendaji wake **Bw.Matiko Mniko**, inaonyesha **Tuzo za Muziki Tanzania** zimejumuisha makundi ya wasanii wa muziki wasioimba kama, watayarishaji wa muziki, wanenguaji na waigizaji kwenye video za muziki. Hivyo basi kutokuimba haiwezi kuwa sababu ya msingi ya kuondoa kipengele cha wasanii aina ya Disco Jokers (Dj's) katika tuzo hizo za muziki.

**Je Disco Jokers(Dj's) sio wasanii wanaotambulika na sheria Tanzania?**

A. Kwa Mujibu wa kifungu cha **17(a)** cha sheria iitwayo **Written Laws(Miscellaneous amendment)Act.no. 5 of 2019** iliyorekebisha kifungu cha 2 cha sheria ya sanaa iitwayo **National Arts Act.no 23 of 1984**, kinatafsiri neno **''Msanii''** kuwa ni mtu yoyote anaejihusisha au kufanya kazi za sanaa

B. Kwa mujibu wa kifungu cha **5(2)(d)** cha sheria ya Hakimiliki iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act.No.7 of 1999(re.2002)** kinatambua na kujumuisha **"muziki"** kwenye orodha ya kazi za sanaa"

Kutokana na maelezo hayo ya sheria, Disco Joker (Dj) anatambulika na sheria kuwa ni "msanii" kwasababu ni mtu Anaejihusisha na kazi za sanaa (muziki)

**Je disco jokers (Dj's) wanahaki ya kushiriki mashindano ya Tuzo za Muziki Tanzania zilizoandaliwa na BASATA?**

Baraza la Sanaa Taifa (BASATA) limeundwa kwa mujibu wa kifungu cha **3(1)** cha sheria ya sanaa iitwayo **National Arts Act.no 23 of 1984,**

Kwa mujibu wa kifungu cha **4(1)(h)** cha sheria ya sanaa iitwayo **National Arts Act.no 23 of 1984,** kimelipa Baraza la Sanaa Taifa (BASATA) majukumu ya kuchochea maendeleo ya kazi za sanaa kwa kuandaa na kupanga maonyesho, matamasha, warsha, semina na mashindano baina ya wasanii.

Tuzo za muziki ni mashindano baina ya wasanii. Disco jokers (Dj's) ni wasanii. Hivyo basi Disco Jokers(Dj) wanahaki ya kushiriki katika Tuzo za Muziki Tanzania.



TARO
TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION

**HITIMISHO**

Kutokana na sheria kuwatambua Disco Jokers (Dj's) kuwa ni wasanii na kuwapa haki ya kushiriki mashindano ya wasanii yanayoandaliwa na BASATA , kitendo cha BASATA Kuwaondoa Disco Jokers (Dj's) kwenye **Tuzo za muziki Tanzania** bila ya kutoa sababu zozote ni **UBAGUZI** kinyume na ibara ya **13(4)** ya **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) kama inavyofanyiwa marekebisho mara kwa mara**, ambayo inaamuru kuwa

*''Ni marufuku kwa mtu yeyote kubaguliwa na mtu au mamlaka yoyote inayotekeleza madaraka yake chini ya sheria yoyote au katika utekelezaji wa kazi au shughuli yoyote ya Mamlaka ya Nchi''*

Kwa mara nyingine TARO tunalaani vitendo vya **KIBAGUZI** vinavyofanywa na Baraza la Sanaa Taifa (BASATA) kwa wasanii katika kutekeleza majukumu yao. BASATA wanapaswa kuacha mara moja ubaguzi huo na kurudisha kipengele cha Disco jokers(Djs) katika vinyang'anyilo vya **Tuzo Za Muziki Tanzania.** Pia BASATA wanapaswa kuwajibika kwa kutoa sababu za msingi za kuwaondoa wasanii aina ya Disco Jokers (Djs) kwenye vipengele vya **Tuzo za Muziki Tanzania**

ASANTENI
MUNGU AIBARIKI TANZANIA
MUNGU ATUBARIKI WATANZANIA
(Kazi iendelee)

Wako katika kujenga Taifa

**Mkurugenzi Mkuu wa Utawala**
**WAKILI JOSHUA MSAMBILA**